THIRDWAY HEADQUARTERS
Chalbi Drive 57, Lavington, P.O. Box 4781-00100 Nairobi
Email: thirdway@thirdwayalliance.com
Website. www.thirdwayalliance.com
Tel. +**254 798013750/49/48**

MSWADA WA MAREKEBISHO YA KATIBA WA PUNGUZA MIZIGO

MPANGILIO WA VIFUNGU

UTANGULIZI

Wito wa Chama cha Third Way Alliance wa kuandaliwa kwa kura ya maamuzi, almaarufu Punguza Mizigo, una lengo moja kuu: kufanyia marekebisho Katiba ya Kenya ya mwaka 2010 ili kupunguza mzigo na gharama ya uongozi inayowakumba Wakenya. Wito huo unahusisha Kifungu 257 cha Katiba ya Kenya kinachosema kuwa wale wanaopendekeza marekebisho ya Katiba ni sharti wawasilishe kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) sahihi milioni moja za wapigaji kura waliosajiliwa wanaounga mkono pendekezo hilo. Wito huu pia unakariri uhuru wa wananchi wa Kenya katika Kifungu cha Kwanza cha Katiba ya nchi. Wito huu ni tofauti na miito mingine yoyote ya kuandaliwa kwa kura ya maamuzi, ukiwemo mpango wa Bunge unaoendelezwa na baadhi ya wanasiasa. Mpango wa Punguza Mizigo unawapa wananchi kipaumbele. Unatambua kwamba Katiba ni azma ya wengi; wala sio wachache wawe wamechaguliwa au la.

Awamu ya kwanza ya mpango wa Punguza Mizigo ilianza mwezi Aprili mwaka 2018 kwa kutoa wito kwa Wakenya kuunga mkono kupitia kwenye mitandao katika tovuti ya https:thirdwayalliance.com. Awamu hii ilitumia fursa ya takriban

watumiaji milioni 15 wa mitandao ya kijamii. Awamu ya pili ilihusisha ziara kwenye Kaunti mbalimbali ambapo pia watu walihamasishwa kuunga mkono mpango huo kupitia mitandao. Ingawa kampeni hiyo ya Punguza Mizigo tayari imefikisha sahihi milioni moja zinazohitajika, watu zaidi wanaendelea kuiunga mkono.

KWA NINI PUNGUZA MIZIGO? –SABABU

I) HAJA YA KUIMARISHA SENETI NA BUNGE LA TAIFA NA KUPUNGUZA GHARAMA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA BUNGE LA TAIFA KWA:

1. Kushughulikia wasiwasi kuhusiana na idadi kubwa ya Wabunge na kupunguza idadi hiyo kutoka 416 hadi 147 kwa:

a) Kufutilia mbali maeneobunge 290;

b) Kufanya kila mojawapo wa Kaunti 47 kuwa eneo bunge moja kwa minajili ya uchaguzi wa wanachama wa Seneti na Bunge la Taifa;

c) Kumchagua mwanamme mmoja na mwanamke mmoja kwenye Bunge la Taifa na kuwateua wabunge sita pekee maalum kutoka makundi maalum. Hii pia itatilia maanani usawa wa jinsia ili kuhakikisha kwamba kutoka kila mojawapo wa makundi hayo maalum kuna mwanamme na mwanamke mmoja.

d) Kuwachagua maseneta 47 kwa kutumia Kaunti kuwa eneo bunge moja.

Sababu

a) Mbali na pendekezo hili kuungwa mkono na Wakenya wengi kupitia kwenye mpango huo maarufu, ni kweli kwamba kuna uakilishi wa zaidi ya asilimia 400 ikilinganishwa na nchi nyingine zenye idadi kubwa zaidi ya watu. Kadhalika, nchi kama Kenya, ambayo ingali inaendelea na iliyo na

mahitaji mengi haiwezi kumudu gharama ya idadi kubwa ya waakilishi. Kwa mfano, China ina waakilishi 1,200 wa jumla ya **watu bilioni-1.4**; India ina **waakilishi 800** wa jumla ya **watu bilioni-1.3,** nayo Marekani ina waakilishi 335 wa jumla ya watu milioni-350. Hivyo basi haileti maana yoyote kwamba **watu milioni-46** katika nchi maskini inayostawi kama Kenya itakuwa na itamudu gharama ya waakilishi 416 katika Mabunge yote mawili. Gharama ya uakilishi huu imechangia pakubwa katika kiwango cha juu cha mishahara ya kitaifa. Kenya ina matatizo makubwa zaidi kuweza kumudu gharama hiyo. Ndiposa kampeni hii ikaitwa Punguza Mizigo ili kuwapunguzia mzigo walipaji ushuru.

b) Swali kuu ni hili: kati ya maendeleo na huduma mashinani kwa upande mmoja na waakilishi zaidi kwa upande mwingine, utachagua ipi?

2. Kaunti zote 47 za humu nchini ni uakilishi tosha wa Wakenya. Magavana huchaguliwa katika kaunti hizi zote pamoja na waakilishi wa wadi, kuwa waakilishi wa watu. Kadhalika, maafisa wakuu wa Kaunti wanaohudumu katika serikali za kaunti ni ngazi nyingine ya uakilishi. Hivyo basi, hatuhitaji kuwapeleka waakilishi zaidi kutoka kwa kaunti hadi kiwango cha kitaifa. Vile vile, kila kaunti humu nchini inaakilisha kabila kuu na lenye idadi kubwa zaidi ya watu katika kaunti hiyo. Hii inamaanisha kwamba kaunti zimekomesha hali ya kihistoria ya kutengwa kwa baadhi ya makabila katika uongozi. Vile vile, kila kaunti kwa sasa inapokea ugavi sawa wa mapato ya kitaifa. Hakuna kaunti au kabila lolote sasa linaloweza kudai kwamba limetengwa. Wanaweza tu kulaumu uongozi duni katika kaunti zao.

3. **Kuifanya kila kaunti 47 kuwa eneobunge kwa minajili ya uchaguzi wa Ubunge wa Seneti na ule wa Taifa. Hatua hii itafutilia mbali maeneobunge 290 yaliyoko.**

Sababu/vigezo

a) Bunge litakuwa na idadi ndogo ya wabunge ambao watakuwa na muda wa kutosha wa kuchangia kwenye mijadala. Kadhalika itahakikisha utenda kazi bora bungeni. Kwa kweli, mpango wa Punguza Mizigo umeungwa mkono na wabunge kadhaa wanaopendelea bunge lenye idadi ndogo ya wabunge badala ya lile la sasa lenye idadi kubwa zaidi. Wabunge wengi walikiri kwamba hawawafahamu wengi wa wenzao bungeni. Bunge lenye idadi ndogo ya wabunge litatenda kazi kwa njia bora zaidi na kuwapunguzia Wakenya gharama;
b) Maeneobunge machache yatahakikisha idadi ndogo ya waakilishi na hivyo kupunguza gharama;
c) Hii itapunguza gharama ya kuendesha shughuli za bunge ambapo rasilimali hizo zitaweza kutumika zinakohitajika zaidi hasa katika kiwango cha kila Wadi ambapo tutaweza kukadiria maendeleo.;
d) Itakomesha ushindani usiofaa baina ya wabunge na waakilishi wa Wadi katika usimamizi wa Wadi hizo;
e) Hii itafanikisha uratibu, uakilishi na usimamizi bora wa Wabunge. Wabunge sasa watafahamu jukumu lao vyema zaidi na kwa mtazamo wa kitaifa badala ya ule wa eneobunge.

3) Pandisha Seneti ngazi kuwa Bunge la Juu lenye mamlaka ya turufu. Hii itahakikisha kwamba Bunge la Taifa linatathminiwa.

Sababu:

a) Hii itaimarisha mamlaka ya Seneti ya kuchunguza maamuzi ya Bunge la Chini (Bunge la Taifa) jinsi ilivyo kwenye maeneo mengine duniani. Bunge la Seneti jinsi lilivyo sasa ni la kufedhehesha. Halina mamlaka ya kupinga baadhi ya sheria zisizofaa zinazopitishwa katika Bunge la Taifa. Kwa mfano, sheria ya ushuru ziada wa thamani (VAT) ya mwaka 2013 ilipitishwa kwa haraka bila kutilia maanani maslahi ya kijamii na kiuchumi ya Wakenya wengi. Ilihusisha zaidi uaminifu kwa chama badala ya wananchi waliowachagua wabunge hao kuwaakilisha. Mfano mwingine ni kupitishwa kwa Sheria kuhusu Ugavi wa Mapato (nambari 7) ya mwaka 2018 ambayo ilikiuka katiba ikizingatiwa kanuni za Kikatiba zinazobainisha kwamba mapato yanafaa kugawa kuambatana na akaunti zilizokaguliwa hivi punde zaidi. Seneti haingeweza kupinga sheria hizo mbili kwani haina mamlaka hayo. Kadhalika, iwapo Seneti ingekuwa na mamlaka hayo ingehoji uamuzi wa Bunge la Taifa wa kupinga ripoti kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa madini ya zebaki kwenye sukari iliyoagizwa kutoka nje.
b) Hii itatoa mpangilio wa bunge utakaohakikisha ubora na tathmini miongoni mwa waakilishi wetu waliochaguliwa. Seneti itaweza kuchunguza maamuzi ya bunge la chini hasa iwapo na wakati ambapo maamuzi hayo yatakuwa na madhara kwa wananchi jinsi ilivyokuwa kwenye ripoti hiyo kuhusu sukari, miongoni mwa nyingine.

Sura zitakazorekebishwa:

a) Sura ya saba: Uakilishi wa watu
b) Sura ya nane: Bunge

II. KUIMARISHA UGATUZI NA KUPELEKA HUDUMA MASHINANI KWA:

4) Kuongeza kiasi cha pesa zinazotengewa kaunti hadi takriban asilimia 35 kutoka asilimia 15 kwa sasa. Wakenya wamo kwenye kaunti, wadi na vijiji.

Sababu/vigezo:

a) Italeta maendeleo ua kiuchumi katika kaunti hasa katika kiwango cha Wadi:
b) Wakenya wako kwenye viwango vya kaunti na wadi; maendeleo mengi yanahitajika katika kiwango cha wadi.kuongeza kiasi cha pesa kwa kaunti kutaharakisha maendeleo; tunataka kuona shule bora, hospitali, barabara, usalama, maji safi miongoni mwa mahitaji mengine katika kiwango cha wadi. Hii ndio njia ya haraka zaidi ya kuwasawazisha Wakenya. Hii itahakikisha kwamba huduma au mashirika ya kiserikali yanaendelezwa hadi kwenye sehemu zote za jamhuri hii kuambatana na Kifungu cha Sita cha Katiba ya nchi.;
c) **Hii itahakikisha ujumuishaji wa wote:** Ujumuishaji maana yake ya kimsingi ni wakati ambapo kila mwananchi anaweza kupata kwa usawa rasilmali za kitaifa. Ugatuzi wa pesa zaidi hivyo basi utahakikisha kwamba kila kaunti au jamii haitahitaji “mtetezi” kupata huduma za umma. Ujumuishaji ukiafikiwa katika kiwango cha wadi, Wakenya wengi hawatajali ni nani anayechaguliwa kuwa Rais. Hii itaiga mfano wa nchi zilizostawi kama Uswizi ambako wananchi hujali zaidi huduma wanazopata. Hii pia itakomesha siasa za kikabila ambazo zimeendeshwa kwa muda mrefu na baadhi ya wanasiasa.

5) Kutumia Wadi kuwa kiwango cha kimsingi cha kuleta maendeleo ya haraka kuchukua mahala pa Hazina ya Ustawi wa Maeneo-bunge CDF, na hivyo kupeleka maendeleo mashinani. Hii itaharakisha ukuaji wa kiuchumi katika kila mojawapo wa Wadi 1450 nchini.

Sababu:

(a) Hii itaharakisha maendeleo ya kiuchumi katika wadi;

(b) Huduma zitaletwa karibu zaidi na wananchi. Hii itaambatana na Kifungu nambari sita (sehemu ya 3) ya Katiba ambacho azma yake ni kumfikia kila Mkenya. Wadi ndio njia bora zaidi ya kuafikia hili.;

(c) Kutumia wadi kama kiwango cha kimsingi cha kuharakisha maendeleo ambapo mfumo wa kuleta maendeleo kuanzia viwango vya mashinani hadi juu ndio utatumika ili kuleta maendeleo sawia katika sehemu zote za nchi. Hii pia inamaanisha kwamba haitajalisha mahali ambako mtu anaishi humu nchini kwani kila Mkenya atapata huduma zote (shule, hospitali, barabara, usalama, n.k.) zinazopatikana kwa wengine iwe ni kwenye maeneo ya mijini au mashambani.

(d) Kuhakikisha wote wanajumuishwa: Kwa kupeleka huduma karibu na mamilioni ya Wakenya, tutakuwa tumeafikia ujumuishaji wa wote. Kwa kutengea kila Wadi pesa za kutosha za kimaendeleo, kila Mkenya atapata huduma sawa za umma. Ujumuishaji huu unaweza tu kuafikiwa wakati kila mwananchi ananufaika wala sio wakati baadhi ya wananchi wananufaika kwa niaba ya eneo, jamii, ukoo au kikundi kingine cha watu.

Sura zitakazorekebishwa:

(a) Sura ya 11: Ugatuzi

(b) Sura ya 12: Fedha za Umma

V. KUKOMESHA UKOSEFU WA USAWA WA KIJINSIA NA KUSHUGHULIKIA KANUNI YA UAKILISHI WA KIJINSIA WA THULUTHI MOJA KATIKA NYADHIFA ZA KIUCHAGUZI.

6. Kukomesha ukosefu wa usawa wa kijinsia uliodumu kwa muda mrefu na kuhakikisha kwamba Wakenya wanamchagua mwanamme mmoja na mwanamke mmoja kutoka kila mojawapo wa Kaunti 47 kwenye Bunge la Taifa. Hii inafutilia mbali wadhifa wa mwakilishi mwanamke.

Sababu:

(a) Kukomesha ukosefu wa usawa wa kijinsia kuhusiana na uongozi na kuafikia usawa baina ya wanaume na wanawake. Kwa muda mrefu, uongozi wa kisiasa umechukuliwa kuwa wadhifa wa wanaume na kila mara wanawake wanapoonyesha azma ya uongozi, wamekumbwa na dhuluma na chuki. Hali hii itakoma kufuatia marekebisho hayo yanayopendekezwa ya Kikatiba. Kenya itasifiwa kwa kuwapa wanawake fursa sawa. Hivyo basi tutakomesha ukosefu wa usawa katika uongozi baina ya wanaume na wanawake.

(b) Hii pia itaafikia usawa wa kijinsia unaotakikana katika uongozi wa kisiasa; na pia kuafikia asilimia 50 kwa 50 ya uakilishi wa kijinsia bungeni. Hii ndio maana sahihi ya usawa.

Sura itakayorekebishwa:

(a) Sura ya nne: Haki za kimsingi

(b) Sura ya nane: Bunge

(c) Sura ya 11: Ugatuzi

III. KUBADILI KIPINDI CHA URAIS NA KUKOMESHA UZUKAJI WA GHASIA ZA KIUCHAGUZI KUTOKANA NA HALI YA RAIS MMOJA KUDUMU WADHIFANI KWA MUDA MREFU

7. Kuanzisha kipindi kimoja cha urais cha miaka saba

Sababu/vigezo

(a) <u>Historia ya ghasia na taharuki za kikabila na kisiasa.</u> Kipindi kimoja kinachopendekezwa cha mwaka mmoja kitakomesha hali ya kupigania kuchaguliwa tena. Kuna mtindo wa ghasia kuzuka wakati wa kila kipindi cha uchaguzi wakati rais aliyepo anapotafuta kuchaguliwa tena. Ghasia hizo ama huzuliwa na rais aliye mamlakani au wapinzani wanaonuia kumwondoa mamlakani. Ghasia za mwaka 1991/1992, 1997, 2007/8 na 2017 hazikuwa sadfa. Ni bayana kwamba hakukuwa na ghasia mwaka 2002 na 2013 na maelezo pekee ni kwamba rais aliyekuwa mamlakani hakuwa akiwania kuchaguliwa tena;

(b) <u>Kuangazia kuchaguliwa tena badala ya utoaji huduma.</u> Historia yetu ya kisiasa imeonyesha kwamba rais anayehudumu kwa mara ya kwanza hutumia mwaka mmoja hadi miwili ya kipindi cha kwanza akiwatuza marafiki wa kisiasa na kumfurahisha kila mtu; kadhalika hakuna lolote linaloafikiwa katika miaka miwili au mitatu ya mwisho kwani rais huangazia kampeni za kuchaguliwa tena au ahadi, ambazo huangazia watu binafsi au kundi la marafiki wa kisiasa. Urais wakati huu hauangazii Mkenya ila marafiki zao wa kisiasa. Hii ni sababu mojawapo ambapo ahadi za kisiasa hazitimizwi katika kipindi cha kwanza na mara nyingi hata katika kipindi cha pili.

(c) **<u>Kukomesha wizi wa pesa za umma.</u>** Wizi wa pesa za umma huongezeka katika miaka miwili ya mwisho ya kipindi cha kwanza cha urais kutokana na haja ya kutafuta kuchaguliwa tena. Kuna mifano mingi ikiwemo hati ya dhamana ya Euro ambayo haikuwajibikiwa, Anglo leasing, sakata ya Goldenberg, ukosefu wa thamani ya pesa ya reli ya kisasa miongoni mwa mengine mengi.

(d) **<u>Kudorora kwa uchumi.</u>** Kipindi kimoja kitakomesha msukosuko wa kiuchumi ulioshuhudiwa kwenye chaguzi za mwaka 1992, 1997, 2007 na 2017. Rais atasalia mamlakani wakati wa kampeni na atakuwa na mamlaka ya kuikinga nchi dhidi ya wawaniaji urais wenye nia mbaya.

(e) **<u>Kupunguza kiwango cha mishahara ya watumishi wa umma.</u>** Wadhifa wa Urais huwa ghali sana na hutumia mabilioni ya pesa za umma. Kipindi kimoja kitaisaidia kuokoa pesa za umma zinazotumika katika chaguzi mbili za urais kila baada ya miaka mitano.

Sura itakayorekebishwa:

(a) Sura ya 9: Serikali Kuu

IV. KUPUNGUZA KIWANGO CHA MISHAHARA NA MATUMIZI YA MARA KWA MARA YA PESA ZA SERIKALI

8. Kupunguza gharama ya kuendesha shughuli za bunge kutoka shilingi bilioni-36.8 kwa sasa hadi chini ya shilingi bilioni-5. Gharama hii basi itakuwa imepunguzwa kwa shilingi bilioni-31.8.

Sababu:

(a) Pesa zitakazopatikana baada ya gharama hiyo kupunguzwa zinaweza kufadhili miradi ya maendeleo katika kaunti na hasa katika kiwango cha Wadi;

(b) Wakenya watapendelea ustawi wa muundo msingi badala ya kutumia mabilioni ya pesa kuwalipa maafisa waliochaguliwa, hali ambayo haiimarishi maisha yao. Kadhalika waakilishi wengi kupita kiasi ni mzigo mwingine wa kifedha. Mbunge mmoja hupokea ruzuku ya kununua gari, mkopo wa kununua nyumba, marupurupu ya kila kikao na marupurupu ya usafiri mbali na mshahara wa takriban shilingi milioni moja. Gharama za usafiri za wabunge ni za juu mno. Huu sio utumiaji pesa za umma kwa hekima.

(c) Pesa zinazotumiwa kwa Bunge ni nyingi sana hasa ikizingatiwa kwamba Kenya bado ni nchi maskini ambayo ingali inang'ang'ana kulipa deni la takriban shilingi trilioni tano. Kiasi cha shilingi bilioni-31.8 zinazoweza kupatikana baada ya gharama hiyo kupunguzwa zikiwekezwa ipasavyo zinaweza kubuni mamilioni ya nafasi za ajira kwa vijana; au kutimiza mikataba kadhaa ya nyongeza ya mishahara ambayo serikali imeshindwa au kukataa kutimiza. Hii itazuia migomo ya wauguzi, madaktari na walimu ambayo husababisha madhara makubwa kwa jamii.

(d) Wakenya bado wanahitaji vifaa vya kimsingi vya kijamii na pesa hizi zinaweza zikatumika kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi ambao wengi wao ni maskini.

9**) Kupiga marufuku nyadhifa maalum katika Mabunge ya Kaunti na Seneti.**

Sababu:

(a) Hii itapunguza gharama ya kuendesha shughuli za Mabunge ya Kaunti na Seneti;

(b) Pesa zitakazopatikana baada ya kukomeshwa kwa matumizi haya yasiyofaa ya pesa zitatumiwa kufadhili miradi ya kimaendeleo au kubuni mamilioni ya nafasi za ajira kwa vijana wasio na kazi.

10. Kukomesha uharibifu wa fedha za umma na kupunguza mishahara ya viongozi waliochaguliwa hadi kiasi cha juu zaidi na malipo ya jumla ya shilingi nusu milioni kwa Rais na shilingi laki tatu kwa kila mbunge kwa mwezi. Viongozi wote waliochaguliwa hawatalipwa marupurupu mengine (marupurupu ya vikao, ruzuku ya kununua gari na mkopo wa kununua nyumba). Tume ya Mishahara na Marupurupu, SRC kuamua mishahara ya viongozi wengine waliochaguliwa.

Sababu:

(a) Ni wazi kwamba viongozi waliochaguliwa wamekuwa wakitumia nyadhifa zao kujinufaisha kibinafsi. Wabunge mara kadhaa na katika siku za awali wameungana kuongeza mishahara na marupurupu yao, kwa mfano, waliongeza malipo yao ya kustaafu kwa asilimia 70. Kufanya kazi katika utumishi wa umma hakufai kutumiwa kama mbinu ya kujitajirisha; kunafaa kuwa huduma kwa jamii. Wale wanaotaka mishahara mikubwa wanafaa kufanya biashara au kujiunga na kampuni.

(b) Wabunge wamekuwa wakipata marupurupu makubwa ya vikao mbali na kuwa waajiriwa wanaopata mishahara. Malipo haya ni wizi uliohalalishwa wa pesa za umma. Utumishi wa umma haufai kuwa vutivu kwa wale wanaotaka kujitajirisha; badala yake unafaa kuwavutia wale wanaotaka kuhudumia jamii.

(c) Nyadhifa za kiuchaguzi zinafaa kuwa kazi za kujitolea ili maafisa waliochaguliwa wasitumie mamlaka waliyopewa ***kujitajirisha*** badala ya kuleta maendeleo;

(d) Viongozi waliochaguliwa walio na ujuzi na uwezo wa kupata mishahara au mapato ya juu kwa mwezi wanaweza kutafuta ajira kwenye kampuni au kufanya biashara;

(e) <u>Kenya inahitaji viongozi wanaowatumikia wananchi.</u> Viongozi waliochaguliwa ni sharti wawe watumishi wa watu. Uongozi unafaa kuwa wito wala sio mbinu ya kujitajirisha.

11. Vunjilia mbali wadhifa wa Naibu Gavana. Gavana amteue miongoni mwa maafisa wakuu wa Kaunti waliosailiwa na kuteuliwa mmoja wao kuwa msaidizi wake mkuu kwa minajili ya utawala. Na iwapo wadhifa wa Gavana utaachwa wazi, Gavana anafaa kuchaguliwa kupitia uchaguzi mdogo.

Sababu:

(a) Manaibu wote wa Magavana hawana majukumu bayana katika Kaunti.

(b) Hii itakomesha taharuki na ushindani wa kisiasa baina ya Gavana na Naibu wake hali ambayo imebainika kuwa inatatiza utoaji huduma na uendeshaji wa shughuli za kaunti;

(c) Hii pia itakomesha tofauti za kisiasa na njama baina ya Naibu Gavana na Gavana kwa upande mmoja, na waakilishi wa wadi kwa upande mwingine. Nyadhifa hizo mbili zimesababisha taharuki ya kisiasa na pia mojawapo wa sababu ambapo Mabunge ya Kaunti yamechochewa kumwondoa Gavana mamlakani.

(d) Hii pia itapunguza kiwango cha mishahara ya wahudumu katika kaunti pamoja na gharama zote zinazohusishwa na Naibu Gavana.

12. Tume za Kikatiba ziwe na wanachama wasiozidi watano watakaohudumu kwa muda ambao watakuwa wakiandaa vikao iwapo ni muhimu na ambao watapewa marupurupu kwa kila kikao kuambatana na kaununi za Tume ya Mishahara na Marupurupu, SRC.

Sababu:

(a) Hii itapunguza kiwango cha juu cha mishahara kwa wahudumu pamoja na gharama zinazohusiana nayo kama vile usalama, malipo ya kustaafu, magari, usafiri na kadhalika.

(b) Tume za Kikatiba ni sharti zitekeleze huduma kama kampuni za kibiashara au bodi za mashirika ya kiserikali. Makamishna hao wanafaa kuandaa vikao iwapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

(c) Hakuna sababu yoyote ya kuwa na makamishna wanaolipwa mishahara ilhali hawahusiki katika shughuli za kila siku za mashirika husika. Makamishna, sawa na wakurugenzi, wananuiwa kusimamia utekelezaji wa sera na hii haihitaji kuwa wakati wote; tunachohitaji kufanya ni kuimarisha kamati kuu za tume mbalimbali;

(d) Mamilioni ya pesa zitapatikana mara tu hatua hii itakapotelezwa. Pesa hizo zinaweza kutumiwa kufadhili maendeleo na huduma nyingine.

Sura zitakazorekebishwa:

(a) Sura ya nane: Bunge

(b) Sura ya 11: Ugatuzi

(c) Sura ya 12: Fedha za Umma

(d) Sura ya 15: Tume na Afisi Huru

V. DUMISHA UADILIFU, KOMESHA UFISADI NA WIZI WA PESA ZA UMMA.

13. Rekebisha Sura ya 6 ya Katiba ili kuidhinisha mapendekezo kuhusu uchunguzi wa umma na ripoti za ukaguzi na kuwazuia watu wote waliohusishwa na sakata kushikilia wadhifa wowote wa umma au serikali. Hii itakomesha ufisadi na hali ya kutojali sheria.

Sababu:

(a) Kukomesha hali ya kutojali sheria humu nchini;

(b) Kukomesha ufisadi na wizi wa pesa za umma;

(c) Kuhakikisha Wakenya wanapata thamani ya pesa zao katika miradi yote ya umma;

(d) Kuwaondoa maafisa wote wa umma na wa serikali wanaovunja sheria;

(e) Adhabu kali kwa wizi wa pesa za umma na hali ya kutojali sheria

14. Kesi za ufisadi na wizi wa rasilmali za umma kusikizwa na kuamuliwa katika muda wa siku 30 huku rufaa zote zikihitimishwa katika muda wa siku 15.

Sababu:

(a) Hii itaharakisha kesi kuhusu ufisadi na wizi wa pesa za umma na itawapa imani wafanyibiashara na pia wawekezaji ambao wataiona Kenya kuwa

eneo bora zaidi kutokana na adhabu kali kwa ufisadi. Hii inahusisha uongozi bora ambao ndio kivutio kikuu kwa uwekezaji;

(b) Kuzuia ufisadi na wizi wa pesa za umma;

(c) Kuanzisha mahakama maalum za kushughulikia kesi za ufisadi na wizi wa pesa za umma.

15. Kutoa adhabu ya kifungo cha maisha gerezani kwa wale wanaopatikana na hatia ya fisadi na wizi wa pesa za umma. Vilevile,kusiwe na msamaha wa rais au msamaha wa aina nyingine yoyote kuhusiana na kesi hizo.

Sababu:

(a) Wizi wa pesa za umma ni janga la kitaifa lialowanyima Wakenya wengi maendeleo. Wizi wa pesa za umma hasa kutoka kwenye taasisi kama vile hospitali, shule, na kadhalika, imeleta mauaji ya halaiki. Watu kama hao hawahitajiki katika jamii yetu.

(b) Ufisadi na wizi wa rasilmali za umma umekuwa uhalifu wa kitaasisi;

(c) Wizi wa pesa za umma umetatiza maendeleo na kuwanyima Wakenya huduma muhimu kadri miaka inavyopita;

(d) Kutoa adhabu kali zaidi kwa wezi wa rasilmali za umma;

Sura itakayorekebishwa:

(a) Sura ya 6: Uongozi na Uadilifu

IV. PUNGUZA GHARAMA YA KUANDAA UCHAGUZI NA USAJILI WA WAPIGAJI KURA.

16. Kila Mkenya aliyefikisha umri wa miaka 18 na ambaye anahitaji kitambulisho cha kitaifa anafaa kuchukuliwa kuwa mpigaji kura aliyesajiliwa kikamilifu kwa minajili ya chaguzi na kura za maamuzi.

Sababu:

(a) Hii itawapunguzia Wakenya na tume ya IEBC gharama ya mabilioni ya pesa zinazotumika katika usajili wa mara kwa mara wa wapigaji kura. Ni dhahiri kwamba kitambulisho cha kitaifa na pasipoti ndizo hati zinazotumika zaidi kwenye upigaji kura na wala sio kadi ya usajili wa upigaji kura. Huku mapendekezo ya kufanya upigaji kura kuwa wa kisasa ukiwemo wala sio upigaji kura kwa njia ya kielektroniki pekee, tutakachohitaji ni kuhakikisha kwamba tuna sajili ya kuaminika ya Wakenya pekee itakayojumuishwa kwenye sajili ya kitaifa ambayo tume ya IEBC inaweza kulainisha na mifumo yake kwa minajili ya uchaguzi;

(b) Gharama ya usajili wa wapigaji kura hufikia mabilioni ya pesa kila baada ya miaka mitano;

(c) Hii itakomesha uharibifu wa pesa za umma kwa kuandaa sajili nyingine ya serikali ilhali tayari tuna moja iliyoandaliwa na Shirika la Kitaifa linalowasajili watu.;

(d) Hii pia itasaidia kudumisha hifadhi moja ya takwimu za idadi ya wananchi inayoweza kuimarishwa kwa urahisi ili kutumika kama sajili ya wapigaji kura;

Sura zitakazorekebishwa:

(a) Sura ya 7: Uakilishi wa Watu

(b) Sura ya 8: Bunge